**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA


Mji wa Serikali
Mtumba,
MtaawaViwanda,
S.L.P 2996,
**40478 DODOMA,**

Simu: +255262963470
Barua pepe: ps@mit.go.tz
Barua pepe: gcu@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz
Faksi +255262963117


## TAARIFA KWA UMMA

## TATHMINI YA MWENENDO WA UZALISHAJI, USAMBAZAJI NA BEI ZA VIFAA VYA UJENZI NCHINI KWA KIPINDI CHA SEPTEMBA - NOVEMBA 2021

---

**Jumatano, 24 Novemba 2021**

Wizara ya Viwanda na Biashara hufanya tathmini ya mara kwa mara ya mwenendo wa uzalishaji, usambazaji na bei za bidhaa muhimu nchini, ikiwemo vyakula, sukari, mafuta ya kula na vifaa vya ujenzi. Taarifa hii inahusu tathmini iliyofanyika kuhusu mwenendo wa uzalishaji, usambazaji na bei za vifaa vya ujenzi, hususan saruji, mabati na nondo katika kipindi cha mwezi Septemba – Novemba 2021. Tathmini ilifanyika katika mikoa tisa inayotumia zaidi bidhaa hizo ikiwa ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Pwani, Shinyanga na Ruvuma.

### *A: Mwenendo wa Bei za Vifaa vya Ujenzi*

### 1. Saruji

Nchi yetu ina viwanda tisa vinavyozalisha saruji vyenye uwezo wa kuzalisha tani 9,080,000 kwa mwaka. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa, katika mikoa iliyofanyiwa tathmini, pamoja na mambo mengine, bei za saruji zimepanda kwa wastani wa shilingi 1,000. Kwa mfano, katika mkoa wa Mwanza bei za saruji imeongezeka kutoka shilingi 19,000 kwa mfuko wa kilo 50 kwa mwezi Septemba 2021 hadi kufikia shilingi 20,000 kwa mfuko kama huo kwa mwezi Novemba 2021. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam, bei zimepanda kutoka shilingi 14,000 kwa mwezi Septemba 2021 hadi shilingi 15,000 kwa mwezi Novemba 2021. Hata hivyo, kwa mkoa wa Ruvuma bei ya saruji ilishuka kwa asilimia 15, kutoka shilingi 17,000 kwa mwezi Septemba 2021 hadi shilingi 14,500 kwa mwezi Novemba 2021.

**2. Mabati**

Nchi yetu ina viwanda vikubwa viwili vinavyozalisha mabati. Vipo pia viwanda vidogo ambavyo hukunja mabati. Kwa pamoja viwanda hivyo vina uwezo wa kuzalisha kwa mwaka mabati 14,949,703 (sawa na tani 200,000), kwa mabati ya *gauge 28* ambayo ndiyo hutumika zaidi. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa bei za mabati *(gauge 28)* imepanda kwa wastani wa asilimia 5.5. Kwa mfano, bei ya mabati kwa Mkoa wa Mwanza imepanda kutoka shilingi 31,700 kwa mwezi Septemba 2021 hadi shilingi 33,400 kwa mwezi Novemba 2021. Kwa mkoa wa Dar es Salaam, bei imepanda kutoka shilingi 28,000 kwa mwezi Septemba 2021 hadi shilingi 29,000 kwa mwezi Novemba 2021.

**3. Nondo**

Nchi yetu ina viwanda 16 vinavyozalisha nondo vyenye uwezo wa kuzalisha tani 1,082,788 za ukubwa mbalimbali *(16mm, 12mm, 10mm na 8mm).* Hata hivyo, kwa sasa viwanda hivi vinazalisha wastani wa tani 750,000 za nondo kwa mwaka. Matokeo ya tathimini yanaonesha kuwa bei za nondo zimepanda kwa wastani wa asilimia sita kati ya Septemba 2021 na Novemba 2021. Kwa mfano, bei za nondo kwa Mkoa wa Mwanza zilipanda kutoka Shilingi 44,000 kwa mwezi Septemba 2021 hadi shilingi 47,500 kwa mwezi Novemba 2021. Bei hizo zilipanda kutoka Shilingi 41,600 kwa mwezi Septemba 2021 hadi shilingi 43,700 kwa mwezi Novemba 2021 kwa mkoa wa Dar es Salaam.

***B: Hatua Ambazo Serikali Inachukua Kudhibiti Ongezeko Lisilohalali la Bei za Bidhaa Muhimu Nchini***

Kwa kuzingatia matokeo ya tathmini hii, mambo mawili ni bayana:-

i.) Kupanda kwa bei za saruji katika kipindi cha tathmini kulisababishwa na mfumo wa usambazaji wa bidhaa hiyo na hakutokani na kupanda kwa gharama za uzalishaji viwandani. Kwa sababu hiyo, ongezeko la bei za saruji katika kipindi tajwa linachukuliwa kuwa halikuwa halali.

ii.) Kuongezeka kwa bei za bidhaa zinazotokana na malighafi ya vyuma (mabati na nondo, nk) kulitokana na kupanda kwa bei za malighafi kutoka nje ya nchi kwa kuwa malighafi za bidhaa hizo kutoka ndani hazitoshelezi.

Katika kukabiliana na upandaji usiohalali wa bidhaa muhimu nchini, Serikali imechukua hatua zifuatazo:

a) Wizara ya Viwanda na Biashara itakuwa ikitoa taarifa ya mwenendo wa wastani wa bei za bidhaa muhimu kila mwezi kwa mikoa yote nchini. Hii itawapa walaji/watumiaji wa bidhaa uelewa wa kutosha kuhusu uhalisia wa bei za bidhaa hizo na hivyo kuwa macho wasilanguliwe na kuwawezesha kutoa taarifa kwa wakati kwa mamlaka husika kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki za kisheria.

b) Tume ya Ushindani imehimizwa kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa upangaji wa bei nchini na kuwachukulia hatua stahiki za kisheria wafanyabiashara ambao wanakiuka Sheria ya Ushindani nchini.

c) Kurekebisha Sheria na Kanuni mbalimbali ili kuruhusu kuingizwa kwa urahisi zaidi malighafi zinazohitajika katika uzalishaji wa bidhaa za vyuma, ikiwemo kuruhusu kuingizwa kwa vyuma chakavu kutoka nje kwa utaratibu utakaohakikisha kuwa bidhaa hiyo inapatikana nchini lakini bila kuathiri afya ya mazingira ya nchi yetu.

d) Serikali imepiga marufuku uuzaji nje ya nchi shaba chakavu *(copper scraps)* na za *ingots* shaba *(copper ingots)* ambazo hutumika sana katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za vyuma nchini.

e) Katika mipango ya muda mrefu, Serikali itatekeleza miradi kielelezo itakayotuwezesha kuzalisha chuma kingi hapa nchini kwa ajili ya viwanda vya ndani na kuuza nje ya nchi.

*Prof.* Kitila A. Mkumbo (Mb.),

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**

## TATHMINI YA UZALISHAJI, USAMBAZAJI NA ONGEZEKO LA BEI ZA VIFAA VYA UJENZI NCHINI

### KIAMBATISHO: MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA ZA UJENZI

**Jedwali Na. 1: Wastani wa bei ya rejareja ya mabati Geji 28 kati ya Septemba 1 na Novemba 15, 2021 (Tshs/Bati)**

| Na.. | Mkoa | Bei Novemba, 2021 | Bei Septemba, 2021 | Tofauti ya Bei |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam | 29,000 | 28,000 | 1,000 |
| 2. | Pwani | 29,000 | 28,000 | 1,000 |
| 3. | Mbeya | 33,000 | 30,000 | 3,000 |
| 4. | Arusha | 33,500 | 32,500 | 1,000 |
| 5. | Kilimanjaro | 33,000 | 32,000 | 1,000 |
| 6. | Shinyanga | 34,000 | 30,000 | 4,000 |
| 7. | Mwanza | 33,400 | 31,700 | 1,700 |

**Jedwali Na. 2: Wastani wa bei ya rejareja ya saruji kati ya Septemba 1 na Novemba 15, 2021 - (Tshs/Mfuko)**

| Na. | Mkoa | Bei Novemba, 2021 | Bei Septemba, 3021 | Tofauti ya Bei |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam | 15,000 | 14,000 | 1,000 |
| 2. | Pwani | 15,000 | 14,000 | 1,000 |
| 3. | Mbeya | 16,500 | 15,500 | 1,000 |
| 4. | Ruvuma | 14,500 | 17,000 | -2,500 |
| 5. | Dodoma | 18,000 | 17,000 | 1,000 |
| 6. | Arusha | 16,500 | 16,500 | 0 |
| 7. | Kilimanjaro | 14,500 | 14,500 | 0 |
| 8. | Shinyanga | 19,500 | 18,500 | 1,000 |
| 9. | Mwanza | 19,000 | 20,000 | 1,000 |

**Jedwali Na. 3 Wastani wa bei ya rejareja ya nondo 16mm kuanzia mwezi Septemba 1 na Novemba 15, 2021 (Tshs/Nondo)**

| Na. | Mkoa | Bei Novemba, 2021 | Bei Septemba, 3021 | Tofauti ya Bei |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam | 43,700 | 41,600 | 2,100 |
| 2. | Pwani | 45,000 | 42,000 | 3,000 |
| 3. | Mbeya | 48,000 | 46,000 | 2,000 |
| 4. | Ruvuma | 45000 | 42,000 | 3,000 |
| 5. | Dodoma | 46,000 | 44,000 | 2,000 |
| 6. | Arusha | 49,500 | 47,000 | 2,500 |
| 7. | Kilimanjaro | 49,000 | 45,500 | 3,500 |
| 8. | Shinyanga | 48,000 | 46,000 | 2,000 |
| 9. | Mwanza | 47,500 | 44,000 | 3,500 |

KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**